TANGAZO LA SERIKALI NA. 161 la tarehe 8/3/2024

SHERIA YA OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA
(SURA YA 430)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 22)*

NOTISI YA UTEUZI WA WAENDESHA MASHTAKA YA MWAKA 2024

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Uteuzi wa Waendesha Mashtaka ya Mwaka 2024.

Uteuzi wa Waendesha Mashtaka

2. Watu ambao majina yao yameainishwa katika Jedwali la Notisi hii wanateuliwa kuwa waendesha mashtaka kwa madhumuni ya kuendesha mashauri ya jinai kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Muda wa Uteuzi

3.-(1) Mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya aya ya 2 atatekeleza jukumu hilo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Notisi hii.

(2) Bila kujali ujumla wa masharti ya aya ndogo ya (1), mwendesha mashtaka aliyeteuliwa chini ya Notisi hii anaweza kutumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha chini ya miaka mitano iwapo ajira ya mtu huyo katika utumishi wa umma itakoma au uteuzi wake utatenguliwa au utasitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

*Tangazo La Serikali Na. 161 (Linaendelea)*

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MAJINA YA WAENDESHA MASHTAKA

| Na. | MAJINA |
|---|---|
| 1. | Adelina Nathanael Yelezwa |
| 2. | Ramadhani Mzee Nyamka |
| 3. | Freedom Philemon Mwakigonjola |
| 4. | Zakayo Eleterius Mlelwa |

Dodoma
12 Februari, 2024

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU
*Mkurugenzi wa Mashtaka*